



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA



02/10/2024

TANGAZO KWA UMMA

KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.

(Limetolewa kwa kuzingatia kanuni 7(1)

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kukopesha vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ambapo jumla ya shilingi **700,000,000/=** zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mkopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo;:-

- I. Kikundi cha Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kiwe kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri.
- II. Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali,
- III. Kikundi cha Wanawake na Vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha Watu Wenye Ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2).
- IV. Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) Mtu Mwenye Ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata Mkopo kama kikundi cha Watu Wenye Ulemavu endapo timu ya Menejimenti ya Halmashauri itajidhihirisha kuwa amekosa Watu wengine Wenye ulemavu, wa kuungana nao katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine.

- V. Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali.
- VI. Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenyewe akili timamu na wenyewe umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea.
- VII. Kikundi cha Vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenyewe umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia Mfumo wa kielektoniki (**tembelea tovuti: <https://mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz>**) ili kutambuliwa na kuomba Mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata au Mtendaji wa Kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo:-

- Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji husika.
- Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo.
- Andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyon dani ya mfumo.
- Taarifa ya akaunti ya benki.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **02/11/2024**.

Tangazo hili limetolewa na: -



Dkt Amon D. Mkoga
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA.

*MKURUGENZI NTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA*